



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



Anwani ya Simu "UCHAGUZI".

Nambari ya Simu: +255 22 2114963-6,

Nambari ya Fkisi +255 22 2116740

Barua Pepe: uchaguzi@nec.go.tz

Tovuti: www.nec.go.tz

(Barua zote za kiofisi ziandikwe kwa
Mkurugenzi wa Uchaguzi)

Unapojibu tafadhali taja:

POSTA HOUSE,
MTAA WA GHANA/OHIO,
S. L. P. 10923,
DAR ES SALAAM.

Kumb. Na. GA 56/167/01/106

20 Januari, 2017

Makatibu Tawala wa Mikoa,
TANZANIA BARA.

YAH : KUKUSANYA MAONI YA WATENDAJI WA UCHAGUZI PAMOJA NA VIONGOZI WA SIASA KUHUSU UGATUAZI WA BAADHI YA MAJUKUMU YA TUME KWENDA OFISI ZA HALMASHAURI

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inategemea kufanya upembuzi yakinifu ambao utahusisha ukusanyaji wa maoni yatakayosaidia kuona ni kwa kiasi gani kuna uhitaji wa baadhi ya majukumu yake kuweza kusogezwa katika Ofisi za Halmashauri. Upembuzi huo utaisaidia Tume kupata picha halisi ambayo itakuwa ndiyo msingi wa maandalizi ya namna ya kutekeleza azma hiyo.


Katika kukusanya maoni, Tume imeandaa madodoso ya aina tatu kwa ajili ya Wasimamizi wa Uchaguzi, Maafisa Uchaguzi pamoja na Viongozi wa Vyama vya Siasa.

Katika kufanikisha zoezi hilo, Tume inawatuma wataalam wake katika Mikoa mbalimbali ambao watakuwa waratibu wakuu wa zoezi hilo. Aidha, watakaohusika kujibu dodoso ni Wasimamizi wa Uchaguzi, Maafisa Uchaguzi. Vile vile Tume inaomba apatikane kiongozi mmoja wa chama chochote cha Siasa ngazi ya Wilaya kwa ajili ya kujibu dodoso linalohusu Vyama vya Siasa.

Zoezi la ukusanyaji wa maoni hayo linatarajiwa kuanza tarehe 31 Januari, 2017.

Tunaomba muwafikishie Wakurugenzi wa Halmashauri wote taarifa hii.

Nawashukuru kwa ushirikiano wenu.



Kailima, R. K

MKURUGENZI WA UCHAGUZI